Ecolebooks.com

SHULE YA UPILI YA KITAIFA YA KAPSABET

Kenya Certificate of Secondary Education

MTIHANI WA MWIGO

102/1 — KISWAHILI —Karatasi ya 1

INSHA

DISEMBA, 2020—Muda: Saa 1 1/2

MWONGOZO

Maagizo

a) *Andika jina lako,nambari ya usajili, mkondo katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
c) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
d) *Kila insha isipungue maneno **400.***
e) *Kila insha ni alama 20.*
f) *Kila insha ni lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
g) *Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
h) ***Karatasi hii ina ~~kurasa 8 zilizopigwa chapa.~~***
i) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

122020

Geuza ukurasa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

1. **Lazima**

Wewe ni mwalimu mkuu wa Shule ya Upili ya Mamboleo. Mwanafunzi wako aliyefanya mtihani wake wa KCSE mwaka jana na kupita vizuri amepewa nafasi katika Chuo Kikuu cha Tumaini. Andika wasifu wake.

i. Hii ni insha ya kiuamilifu.

ii.Wasifu ni maelezo ya kina kuhusu mambo,matendo na tabia za mtu na ambayo huelezwa na mtu mwingine.

SURA YA WASIFU

A. KICHWA/MADA

i. *Mada ianze kwa neno 'wasifu.'*

ii. *Itaje ni wasifu wa nani—Lulu.*

iii. *Iandikwe kwa herufi kubwa kisha kupigiwa mstari.*

iv. *Isiwe na alama nyingine ya uakifishaji kando na mstari***.**

WASIFU WA LULU

Au

WASIFU WA MWANAFUNZI LULU

***B*. UTANGULIZI**

C. MWILI (YALIYOMO)

i. *Iandikwe kwa nafsi ya tatu.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

ii. *Iandikwe kwa wakati uliopita, hali timilifu au pamoja na hali ya kuendelea.*

iii. *Matukio yatiririshwe na mtahiniwa kiwakati.*

102/1

122020 **Geuza ukurasa**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

iv. *Baadhi ya maudhui/masuala yanayostahili kushughulikiwa ni:*

1. *Tambulisha jina la mwanafunzi.*
2. *Elezea alikozaliwa*
3. *Fafanua kuhusu utoto wake; alikokalia na kukua kwake.* ***aya 1***
4. *Elezea kuhusu aila yake/jamaa yake, wavyele wake.*
5. *umri wake*
6. *Tambulisha jinsia yake.*
7. *Elezea kuhusu lugha anazozifahamu.*
8. *Elezea kuhusu masomo yake alipokuwa chekechea—alisomea wapi, ufanisi wake katika kiwango hiki, ushindi wake na pingamizi alizokumbana nazo.*
9. *Elezea kuhusu masomo yake katika shule ya msingi na upili:*
   a. *Alisomea wapi, akiwa na umri upi?*
   b. *Alishiriki katika vyama vipi?*
   c. *Aliingiliana vipi na wanafunzi wenzake: je, aliwasaidia wasiojiweza kimawazo, kifedha?*
   d. *Nidhamu yake?*
   e. *Alileta mchango upi/ushindi wake/tuzo zake/alianzisha mradi upi ambao labda ulichochea ndoto yake ya kuwasaidia wenzake?*
   f. *Alihusiana vipi na walimu wake?*
   g. *Elezea pingamizi alizokumbana nazo na alikabiliana nazo vipi?*
   h. *Alifanya vipi katika mitihani yake; darasa la nane na kidato cha nne?*
   i. *Azima yake baada kuhitimu masomo ya kidato cha nne—kusoma zaidi ijitokeze waziwazi*
10. *tabia zake*
11. *tajiriba zake*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

122020 **Geuza ukurasa**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

D. HITIMISHO

Mtahiniwa ahitimishe kwa kuelezea:

i. umaarufu wa mwanafunzi

ii. sababu za mwanafunzi huyo kuhitaji utambulisho

Lulu amekuwa mfano bora kwa vijana wote vitongojini na mjini. Amekuwa akiwahamasisha wanahirimu wenzake baada ya masomo yake ya kidato cha nne kuhusu umuhimu wa mshikamano mwema. Kwa upande mwingine, amekuwa akiwanasihi vijana kuasi matumizi ya afyuni na ulanguzi wa mihadarati. Hivi majuzi, amekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za watoto kimasomo.

2. Mitandao ya kijamii ina faida na hasara zake. Thibitisha.

i. Hii ni insha ya mjadala.

ii.Mtahiniwa lazima aangazie sehemu zote mbili; faida na hasara.

iii.Mifano ya mitandao ya kijamii—facebook, whatsapp, imo,zoom, wavuti, baruapepe,Instagram,telegram,Twitter,SnapChat,WeChat,Messenger,Pinterst, Youtube,Linkedln

iv. Baadhi ya maudhui ni kama yafuatayo:

FAIDA ZA MITANDAO YA KIJAMII

1. *Hurahisisha mawasiliano/mawasiliano ya haraka na kwa watu wengi.*
2. *Hutoa nafasi za ajira kwa urahisi.*
3. *Huunganisha wanajamii/hukuza umoja wa kitaifa na kimataifa.*
4. *ni njia mojawapo ya kupata burudani*
5. *ugwe wa kukuza vipawa*
6. *Husaidia wasomi katika kufanya utafiti.*
7. *Hutumiwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi.*
8. *Hujenga mahusiano mazuri—ndoa kupitia mitandao*
9. *Huimarisha biashara katika maeneo mbalimbali/kote ulimwenguni.*
10. *Husaidia kupitisha wakati.*
11. *Husaidia kuenea kwa utamaduni, mila, lugha(Kiswahili) kote ulimwenguni.*
12. *ni hifadhi nzuri ya ujumbe, miswada, video na picha*
13. *Baadhi huweza kuwa na kamera.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

122020 **Geuza ukurasa**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

HASARA ZA MITANDAO YA KIJAMII

1. *Imechangia kuongezeka kwa ajali za ndege, meli au za barabarani.*
2. *Imechangia kuzorota kwa maadili kwa sababu zina filamu chafu na picha za ngono.*
3. *Imetumika na matapeli kuwalaghai watu na kuwaibia pesa.*
4. *Imesababisha kuvunjika kwa familia au mahusiano mabaya ya kimapenzi.*
5. *Haina siri—mashirika yanayoimiliki hupokea kila ujumbe.*
6. *Hutumiwa na wanafunzi kuibia mitihani.*
7. *Imeharibu lugha ya watu hasa wanafunzi kisarufi na kimsamiati.*
8. *Huwa na mionzi (aina ya miale yenye sumu) ambayo ni hatari kwa afya ya watumizi.*
9. *Huwa ni ya gharama kali kwa sababu ya kununua kadi/data ya mtandao kila wakati, gharama ya kuongeza moto.*
10. *Hufanya wafanyakazi kuwa watepetevu kazini kutokana na uraibu wa kuitumia.*
11. *Huchangia sana vijana kujiunga na makundi ya kiuhalifu/kiharamu.*
12. *Wasioifahamu/kumudu hupitwa na habari muhimu.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

122020 **Geuza ukurasa**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

3. **Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:**
   Wakosanao ndio wapatanao.
   i. Mtahiniwa atunge kisa kinachoonyesha ukweli wa methali hii.
   ii.Kisa kibebe sehemu mbili ya methali:
   a. *Wakosanao—mtahiniwa aangazie wahusika ambao wametofautiana/ wana mzozo na kuwa maadui*
   b. *Ndio wapatanao—wahusika waliokuwa na mzozo/waliotofautiana/maadui wanakuja kupatana/kusuluhisha matatizo yao/tofauti zao kisha kuishi kama marafiki au wasameheane.*

4. **Andika kisa kinachomalizikia kwa kauli ifuatayo:**
   ...Tangu siku hiyo kijiji kizima kilipata funzo kwamba umdhaniaye ndiye kumbe siye na umdhaniaye siye kumbe ndiye.
   i. Mtahiniwa atunge kisa kinachooana na mdokezo huu.
   ii.Kisa kimalizike kwa maneno haya.
   iii.Kisa kilete maana ya kauli kwamba umdhaniaye ndiye kumbe siye na umdhaniaye siye ndiye.
   iv. *Insha hii ina sehemu mbili: mtu/mhusika aliyedhaniwa vibaya/vizuri baadaye aonekane kama mzuri au mbaya.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

122020 **Geuza ukurasa**

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM